Nini Maana Ya Kujipamba Kwa Kujisitiri?

na

Ellis P. Forsman

Nini Maana Ya Kujipamba Kwa Kujisitiri?

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 17, 2011

Nini Maana Ya Kujipamba Kwa Kujisitiri?

1 Tim. 2:9-10

Kila mila inafunua mtazamo wake wa kujisitiri kwa upande wa mavazi:

Baadhi ya mila – kutoka katika mtazamo wetu wa magharibi – haijali kitu kutokana na swala hili.

Mila zingine – kama mtazamo wetu wa magharibi – inakiwango, lakini inatofautiana kutoka kizazi kimoja hadi kingine; mkoa hadi mkoa; mtu na mtu.

Bado mila zingine – zinatofautiana "na yetu" – haionekani ikibadilika bali inaonekana zaidi kuwa kali.

Kama ilivyotazamwa hapo juu "mtazamo" ikiwa upande wa mila, hii inachanganya:

Je mila inatawala kujipamba au kutokujipamba ukizingatia mavazi yetu?

Kama mila inatawala: je hii haiwezi kusemwa kwa mila inayotawala kinachoanzisha ndoa, au kinachoanzisha wizi, au kinachoanzisha ubatizo?

Ukweli wa Mungu, kwa upande mwingine, maranyingi si rahisi kukubali, lakini iko wazi: ukiunganisha na juu ya kinachoanzisha kujipamba kwa kujisitiri ukizingatia mavazi yetu.

Neno la Mungu ni "*taa ya miguu* (yetu)" (Zab. 119: 105) tunapolipokea kwa utayari wote.

Matendo. 17:11, "*Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.*"

Mioyo mizuri na waungwana zitajifunza ili kujionyesha kuwa zimekubaliwa na Mungu, zikitumia kwa halali neno la kweli.

- Luka 8:15, "*Na zile penye udongo mzuri, ndio wale ambao kwa unyofu na wema wa mioyo yao hulisikia neno, na kulishika; kasha huzaa matunda kwa kuvumilia.*"
- 2 Tim. 2:15, "*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.*"

Katika somo hili tunakwenda kuangalia:

- Viwango vya mwanadamu kwa kuzingatia kinachoanzisha kujipamba kwa kujisitiri.
- Neno la Mungu lililofunuliwa kwa kuzingatia kiwango cha kujisitiri.
- Tukichukua kiwango hicho na kukiweka katika mavazi yetu.

Kweli: Kiwango cha mwanadamu kwa kuzingatia mapambo imetapakaa na inachanganya

Kwa ajili ya kidunia:

Mitha. 14:12, "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti."

Mtu anaweza kufikiria *haipendezi* kwenda kufungua mlango akiwa katika nguo ya ndani, lakini akafiria *inapendeza* kuvaa "nguo hiyo iyo" katika umati wa watu.

Mwingine anaweza kufikiria kuwa inapendeza kuvaa nguo "inayoonyesha viungo vya ndani" lakini ni sawa kuvaa nguo iliyombana.

Kufikiria kwa namna hii hakuwezi kuegemea katika ufunuo wa neno la Bwana, lakini kibinafsi/ jamii inatawala viwango vyao vya mamlaka.

Fikra za kidunia na viwango vimeingia katika Kanisa la Bwana.

Idadi kubwa ya Wakristo wameiga viwango vya dunia. Wengine wanajifunza juu ya swala hili lakini wanakata kuruhusu vifungu vya wazi kuongoza uelewa wao.

Matokeo: Amawatumie kanuni ambazo zina zinafunua ukweli wa biblia juu ya swala hili.

2 Petr. 3:17-18, "*Basi wapenzi mkitangulia kujua hayo, jilindeni nafsi zenu, msije mkachukuliwa na kosa la hao wahalifu mkaanguka na kuuacha uthibitifu wenu. Lakini kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele.*"

Kweli: kiwango cha Mungu cha Kujisitiri inaeleweka

Kumbuka: Kuna wengine walio na hali mbaya, na utupu ndiyo matokeo ya umasikini wao.

- Kumbu. 28:47-48, "*Kwa kuwa hukumtumikia BWANA, Mungu wako, kwa furaha na moyo wa kushukuru kwa ajili ya ule wingi wa vitu vyote; kwa hiyo utawatumikia adui zako atakaowaleta BWANA juu yako, kwa njaa, na kwa kiu, na kwa uchi, na kwa uhitaji wa vitu vyote; naye atakuvika kongwa la chuma shingoni mwako, hata atakapokwisha kukuangamiza.*"
- Ezek. 18:5-9, "*Bali kama mtu ni mwenye haki na kuyatenda yaliyo halali na haki; hakuna juu ya milima, wala hakuviinulia macho vinyago vya nyumba ya Israeli wala hakumtia unajisi mke wa jirani yake, wala hakumkaribia mwanamke wakati wa kutengwa kwake; wala hakumdhulumu mtu, bali amemrudishia mdeni wake rehani yake, wala hakumnyang'anya mtu mali yake kwa nguvu, naye amewapa wenye njaa chakula chake, na kuwavika nguo walio uchi; ambaye hakumkopesha mtu ilia pate faida, wala hakupokea ziada ya namna yo yote; naye ameuepusha mkono wake na uovu, na kufanya hukumu ya haki kati ya mtu na mwenzake; tena ikiwa amezifuata sharia zangu, na kuzishika hukumu zangu; mtu huyu ni mwenye haki; hakika ataishi asema Bwana MUNGU."*

Kama hii SIYO dhambi

Yafuatayo haihusiani na mambo ya umasikini, bali mambo ya uwezo na uchaguzi kupitia utajiri ambao Mungu wetu ametupatia

Au somo hili halifikii tu katika uchi, bali kila mmoja anaye endana na neno "pambo."

Uchi uliyotafsiriwa katika kanuni la neno la Mungu.

Kabla dhambi haijaingia ulimwenguni: Adamu na Eva walikuwa uchi... na walikuwa HAWANA aibu.

Mwanz. 2:25, "*Nao walikuwa uchi wote wawili, Adamu na mkewe, wala hawakuona haya.*"

Baada ya dhambi kuingia ulimwenguni, wote walijua kuwa walikuwa uchi na wakatengeneza "vazi" katika jaribio la kujifunika uchi wao.

Mwanz. 3:7, "*Wakafumbuliwa macho wote wawili wakajijua kuwa wa uchi, wakashona majani ya mti, wakajifanyia nguo.*"

Wakajifunika vibaya, wote (walikuwa na hofu) kwa sababu walikuwa uchi.

Mwanz. 3:8-10, "*Kisha wakasikia sauti ya BWANA Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, BWANA Mungu asiwaone. BWANA Mungu akamwita Adamu, akamwambia Uko wapi? Akasema nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha.*"

Mungu aliwavisha kwa mavazi ya ngozi (koti refu: ambayo inamaanisha "funika").

Mwanzo 3:21, "*BWANA Mungu akawafanyia Adamu na mkewe mavazi ya ngozi, akawavika.*"

Makuhani walikuwa wanavaa makoti marefu hadi chini ili kufunika uchi wao, kufunika kwanzia kiunoni hadi mapajani.

- Kutoka 20:26, "*Tena hutapanda kwenda madhabahuni kwangu kwa daraja, uchi wako usidhihirike juu yake.*"

- Kutoka 28:40-42, "*Kisha utafanya kanzu kwa ajili ya wana wa Haruni, nawe wafanyie mishipi, wafanyie na kofia kwa utukufu na uzuri. Nawe mvike huyo nduguyo Haruni na wanawe nao mavazi hayo; nawe watie mafuta na kuwaweka kwa kazi takatifu, na kuwa takasa, ili wapate kunitumikia mimi katika kazi ya ukuhani. Nawe wafanyie suruali za nguo za kitani, ili kufunika tupu ya miili yao; suruali hizo zitafika tangu kiunoni hata mapajani.*"

Maelezo ya kimwili kuhusu "Uchi" inasaidia kuelewa kiini cha *uchi* ilitumika kuonyesha dhambi zao.

Isaya 20:4, "*Vivyo hivyo mfalme wa Ashuru atawachukua uchi, wafungwa wa Misri na watu wa Kushi waliohamishwa, watoto kwa wazee, hawana viatu matako yao wazi, Misri iaibishwe.*"

Kujisitiri inavyofafanuliwa na kanuni iliyofunuliwa katika neno la Mungu.

- 1 Tim. 2:9-10, "*Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi, si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za dhahabu; bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu.*

- 1 Petr. 3:1-4, "*Kadhalika ninyi wake watiini waume zenu, kusudi ikiwa wako wasioliamini Neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake zao, pasipo lile Neno; wakiutazama mwenendo wenu safi, na wa hofu. Kujipamba kwenu kusiwe kujipamba kwa nje, yaani kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi; bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika, yaani roho ya upole na utulivu, iliyo na dhamani kuu mbele za Mungu.*"

Pamoja na adabu nzuri na moyo wa kiasi (si kwa kusuka nywele wala kwa dhahabu na lulu wala kwa nguo za dhahabu).

Kifungu hiki kinasisitiza muonekano unaoonekana katika ubora wa uungu ambao utajionyesha wenyewe ukilinganisha na ule mtindo wa ulimwengu.

Msisitizo ni wa kiungu, na siyo wa kidunia.

Muhtasari:

Tabia za kujisitiri ni pamoja na - ungwana, upole, usitarabu, kujipamba, adabu nzuri, moyo wa kiasi.

Ni uungwana, adabu nzuri tabia ambazo ni nzuri zinazojionyesha zenyewe pamoja kama mavazi.

Matunda yako yanaonyesha kiwango chako cha kujisitiri

Mtu anajulikana kwa matunda yake.

Mathayo 7:15-20, "*Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali. Mtawatambua kwa matunda yao. Je! Watu huchuma zabibu katika miiba au tini katika mibaruti? Vivyo hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri na mti mwovu huzaa matunda mabaya. Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya wala mti mwovu kuzaa matunda mazuri. Kila mti usiozaa tunda zuri hukatwa ukatupwa motoni. Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua.*"

Mtu ambaye anajisitiri kwa mavazi yasiyofaa anazaa matunda ya ulimwengu.

Mtu anayejisitiri kwa mavazi yanayofaa (pamoja ikisaidiwa na utuwema iliyoonyeshwa kwanza) huzaa matunda ya Rohoni.

Matunda yako pia yanaonyesha kiwa unachoishi kwalo:

Je inategemea viwango vya mwanadamu?

Wagal. 5:19, "*Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu,, hasira, fitina, faraka, uzushi.*"

Au inategemea juu ya kiwango cha Mungu?

Wagal. 2:22-23, "*Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sharia.*"

Mwishoni, utavuna (uharibifu) ambacho ulipanda (katika mwili).

Wagal. 6:7-8, "*Msidanganyike Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye katika mwili wake, katika mwili wake atavuna aharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele.*"

Mwisho

Wakati kiwango cha mwanadamu juu ya kutokujisitiri (au somo lolote) siyo sahihi na inachanganya, kiwango cha Mungu ni nzuri na wazi: kutokujisitiri vizuri ni aibu na ni dhambi.

Jijaribuni wenyewe kuona kwamba mpo "katika imani" ukizingatia swala hili.